# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 017

JULAI - SEPTEMBA, 2022


## Serikali imejipanga kutoa huduma kwa wananchi-Mhe. Samia





## Waharibifu wa vyanzo vya maji wachukuliwe hatua - Mhe. Samia




*"Serikali itaendelea kuhudumia wananchi kwa nguvu zote wapate huduma ya majisafi" Mhe. Samia amesema na kuongeza yeye kama mama anaelewa adha wanayopata akina mama inapotokea upungufu wa maji hivyo mradi huo umeondosha hali hiyo katika jamii.*

# Serikali imejipanga kutoa huduma kwa wananchi-Mhe. Samia



**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa majisafi wa Makongolosi, Chunya mkoani Mbeya ambao umeboresha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi wa eneo hilo na kusisitiza Serikali imwejipanga kutoa huduma kwa wananchi wake.

Mhe. Samia akiongea na wakazi wa Chunya katika uwanja wa Shule ya Makongolosi, Kata ya Bwawani amesema serikali inatumia fedha nyingi ili wananchi wapate huduma bora ya maji ambapo mradi huo umewezesha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 10 hadi asilimia 70.

“Serikali itaendelea kuhudumia wananchi kwa nguvu zote wapate huduma ya majisafi” Mhe. Samia amesema na kuongeza yeye kama mama anaelewa adha wanayopata akina mama inapotokea upungufu wa maji hivyo mradi huo umeondosha hali hiyo katika jamii.

Ameongeza kuwa mradi wa maji wa Makongolosi utazalisha maji kiasi cha lita milioni moja na nusu, zaidi ya mahitaji ya sasa ambayo ni lita milioni moja nukta mbili. Pamoja na hilo, Amesesitiza hali itazidi kuwa nzuri kwa sababu mkoa wa Mbeya una jumla ya miradi ya maji ipatayo 50.

Katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga amesema kinachoendelea hivi sasa katika mradi huo ni pamoja na kuwaunganishia wananchi huduma ya maji katika makazi yao

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua mradi wa majisafi wa Makongolosi, Chunya mkoani Mbeya*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua mradi wa majisafi wa Makongolosi, Chunya mkoani Mbeya*

# Waharibifu wa vyanzo vya maji wachukuliwe hatua - Mhe. Samia



*Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza na wakazi wa Mbalizi, jijini Mbeya mara baada ya kuzindua mradi wa maji wa Shongo – Mbalizi.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa maji wa Shongo-Mbalizi, mkoani Mbeya na kuwataka wananchi kulinda mazingira, pamoja na vyanzo vya maji.

Mhe. Rais akiongea na wakazi wa Mbalizi amesema serikali inaweka fedha nyingi katika miradi ya maji ili wananchi wapate huduma ya majisafi, na hivi sasa wananchi wameona hali ya tofauti ya huduma ya maji awali kabla ya mradi na sasa ambapo maji yanapatikana kwa asilimia 95.

“Yeyote atakayeharibu chanzo cha maji achukuliwe hatua stahiki” Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema na kuongeza ni wajibu wa viongozi na wananchi kulinda vyanzo vya maji ili miradi itoe huduma ya maji wakati wote.

Ameagiza maji yanapokatika kutokana na dosari yoyote wananchi wapewe taarifa mapema na sio watendaji kukaa kimya bila kueleza kinachoendelea katika huduma ya maji.

Awali akiongea katika hafla hiyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga amesema mradi huo utahudumia wakazi wapatao elfu 80 na unazalisha lita milioni 8.1 kwa siku.

Wananchi watakaonufaikana na mradi huu mkubwa katika eneo la Izumbwe ni kutoka maeneo ya Mbalizi, Nsalala, Songwe, Mlima wa Reli, Mapelele, Izumbwe na Jeshini na kutoa fursa kwa wananchi wa maeneo hayo kutumia muda wa kutosha kufanya shuguli za kiuchumi badala ya kutafuta maji.

Wizara ya Maji imefanya utekelezaji wa mradi huu kwa miezi 12 kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya WSSA), kwa thamani ya shilingi bilioni 3.3 ikiwa ni sehemu ya kuzidi kuimarisha huduma za majisafi nchini.

# Mradi wa Sibwesa wazinduliwa




*Hafla ya uzinduzi wa mradi wa maji wa Sibwesa*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amezindua mradi wa maji wa Sibwesa wilayani Tanganyika Mkoani Katavi.

Mradi huu ni sehemu ya ufanikishaji wa Kampeni ya Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 katika sekta ya maji na umegharimu milioni 173.2.

Mhe Dkt. Mpango ametumia wasaa wa uzinduzi wa mradi kuipongeza Wizara ya Maji kwa kusimamia utekelezaji wa mradi huo na kusisitiza iendelee kujipanga zaidi ili chanzo cha uhakika cha maji ya Ziwa Tanganyika kitumike kwa ajili ya huduma ya maji katika mkoa wa Katavi.

Awali akiongea katika hafla hiyo Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema mradi huo utaongezwa zaidi ambapo shilingi bilioni 1.8 zimetengwa kwa kazi hiyo na mkandarasi ameshapatikana. Amesema lengo la Wizara ni kuhakikisha wananchi wa Sibwesa, na taasisi zote zilizoko katika eneo la mradi wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.



# Aweso ajiridhisha utoshelevu wa maji Bwawa la Mtera




Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amefika katika Bwawa la Maji la Mtera na kujiridhisha na kiwango cha maji kilichopo katika Bwawa hilo.

Mhe. Aweso amefanya ziara hiyo kuona uhalisia na utoshelevu wa maji katika bwawa hilo kutumika kama chanzo cha ziada ya huduma ya maji katika jiji la Dodoma akiwa na wataalamu wa sekta mtambuka.

Amesema Jiji la Dodoma linaweza kuwa na chanzo cha maji zaidi ya kimoja, na maji yanayoweza kuchukuliwa katika bwawa hilo ni zaidi ya lita milioni 133, ambayo yatahudumia wakazi wa Dodomaa mbapo Bwawa la Mtera lina uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo milioni 3,700 likijaa.

" Maji isiwe sababu ya kukwamisha maendeleo ya wananchi wa Dodoma na nchi yetu" Waziri Aweso amesema na kuongeza atafanya kikao na Waziri wa Nishati ili kuona namna bora ya kuwasaidia wakazi wa Dodoma katika mpango huo wa muda mfupi wa kutumia Bwawa hilo kama chanzo cha maji.

Amefafanua kuwa mpango wa muda mrefu ni kutumia maji kutoka ziwa Victoria ili yatumike katika shughuli mbalimbali za kiuchumi jijini Dodoma, kwa sababu hivi sasa mahitaji ya maji ni lita milioni 133, na yanayozalishwa ni lita milioni 67, hivyo Dodoma ina upungufu wa lita milioni 66 na kama viongozi wanalojukumu la kufanyia kazi.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji Bw. Florence Mahay amesema wao kama bonde wanasimamia rasilimali za maji ipasavyo, na maji yatakayochukuliwa katika Bwawa la Mtera hayatakuwa na madhara katika kazi ya kuzalisha umeme kwa sababu yatakuwa asilimia moja ya maji yanayotumika katika kazi hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) akiongea katika ziara hiyo amesema ongezeko la watu limekuza mahitaji ya huduma ya maji, na mradi wa kuongeza maji kutoka Bwawa Mtera utafikisha jumla ya lita milioni 201 ambazo zitaweza kutumika kwa miaka 13 ijayo jijini Dodoma.

Pamoja na hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri amepongeza hatua yakuwa na vyanzo zaidi ya kimoja kwa huduma ya maji, na kusisitiza maji ni muhimu katika maeneo mtambuka kuanzia makazi hadi katika miradi mikubwa, viwanda na mifugo.

# Serikali kumaliza upungufu wa Huduma ya Majisafi Mwanza

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango amesema Serikali imedhamiria kuwaondolea adha ya maji wananchi wa Jiji la Mwanza kwa kujenga miradi mikubwa ya huduma ya majisafi inayotumia chanzo cha maji cha ziwa Victoria.

Ameyasema hayo hivi karibuni wakati wa hafla ya Uwekaji wa Jiwe la Msingi la Mradi wa Ujenzi wa dakio jipya la maji katika eneo la Butimba Jijini Mwanza, ujenzi ambao utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 69.

Ameelekeza mradi huo ukamilike ifikapo Noeli ya mwaka 2022, iwe zawadi ya wakazi wa jiji la Mwanza wakati wa sherehe hiyo. Pamoja na hilo ameelekeza wananchi wanaoishi karibu na mradi huo wapewe kipaumbele katika kupata huduma ya majisafi na kuunganisha huduma ya maji isizidi siku saba.

"Serikali inatambua kasi ya ukuaji wa Jiji la Mwanza pamoja na changamoto ya upatikanaji wa majisafi katika baadhi ya maeneo ya pembezoni na yale yenye miinuko mikali, mradi huu kwa kiasi kikubwa utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo mengi," Mhe. Dkt. Mpango amesema.

Amebainisha kuwa mradi huo utakapokamilika utahudumia wakazi zaidi ya 450,000 na kukamilika kwake kwa kiasi kikubwa kutapunguza changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa Mwanza.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan inaendelea na jitihada za dhati za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini. Serikali inatekeleza miradi hii ili kuhakikisha huduma za msingi za kijamii zinapatikana kwa wananchi wote," amesema.

Mhe. Dkt. Mpango ameyataja maeneo yakayaonufaika na mradi huo kuwa ni pamoja na Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Lwanhima, Fumagila, Sahwa, Igoma, Kishiri na Nyamhongolo. Aidha amesema maeneo ya Usagara, Nyashishi na Fella katika Wilaya ya Misungwi pamoja na maeneo ya Kisesa, Bujora na Isangijo katika Wilaya ya Magu pia yatanufaika.

Awali, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akizungumza katika hafla hiyo amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, huduma ya maji kwa maeneo ya mijini inafika asilimia 95 na maeneo ya vijijini asilimia 85.

Amesema Wizara inatambua kuwa Jiji la Mwanza linakuwa kwa kasi na kwamba pamoja na mradi huo kuzalisha lita za ujazo milioni 48 kwa siku, Serikali kwa kushirikiana na wadau wake wa kimaendeleo itaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya mradi huo pamoja na uboreshaji wa chanzo cha Maji cha Capripoint ili kiweze kutosheleza mahitaji kwa Jiji la Mwanza ambalo kwa sasa linahitaji lita milioni 160 kwa siku.

"Natambua kazi kubwa inayofanywa na Mamlaka ya Majisafi Mwanza (MWAUWASA), wanapambana usiku na mchana katika kuhakikisha huduma ya maji inakuwa nzuri," Mhe. Aweso amesema wakati akizungumzia hali ya huduma ya majisafi jijini Mwanza.

Mhe. Aweso (Mb) amebainisha kuwa Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya majisafi nchini yenye lengo la kuhakikisha huduma ya Majisafi, salama na yenye kutosheleza inawafikia wananchi wote.




***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango pamoja na viongozi wengine mara baada ya kuweka jiwe la msingi la dakio jipya, Butimba, Jijini Mwanza.***

# TANZANIA MWENYEKITI BONDE LA MTO NILE




**Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), kushoto, akiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mpito ya Nile (NBI), Bw. Sylivester Matemu, jijini Dar es salaam.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo ametoa wito wa kulinda rasilimali za Bonde la Mto Nile ili zilete manufaa kwa wananchi wanalolizunguka. Jafo ametoa wito huo akifungua mikutano ya Baraza la Mawaziri wa Bonde la Mto Nile akimwakilisha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango katika Hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es Salaam. Tanzania imepokea uenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile katika kikao hicho.

Waziri Jafo amesema ushirikiano ni njia bora katika kusimamia kwa amani rasilimali za maji, hivyo mikutano ya Mawaziri wa Bonde la Mto Nile inatoa fursa ya kutafakari na kufanya kazi pamoja na kuweka misingi ya ushirikiano na kutoa maelekezo ya kisera kuhusu usimamizi wa rasilimali hiyo.

Amesema hadi sasa kuna zaidi ya Mabonde ya majishirikishi 276 duniani likiwemo Bonde la Mto Nile, ambayo yanachukua nusu ya ardhi ya dunia na kukaliwa na watu zaidi ya bilioni 3 ambao ni kiasi cha asilimia 40 ya watu wote duniani.

Katika hatua nyingine, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekabidhiwa uenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile kwa mwaka 2022/2023 katika mikutano ya Mabaraza ya Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile katika Hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amepokea uenyekiti huo kutoka kwa mwakilishi wa Waziri wa Umwagiliaji na Rasilmali za Maji wa Sudan ya Kusini, Balozi wa Sudan Kusini nchini Tanzania, Mhe. Deng Majok ataliongoza baraza hilo lenye wanachama wa nchi 10 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Nile Basin Initiative (NBI), Sylivester Matemu amesema ushirikiano huo umekuwa na manufaa makubwa kwa nchi zote 10 zinazounda Bonde la Mto Nile.

Baraza la Mawaziri kupitia kikao hicho limepitisha Mpango wa Usimamizi wa Bonde la Mto Nile unaolenga kutoa mwongozo katika upangaji na utekelezaji wa shughuli za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde la Mto Nile kwa ngazi ya kitaifa na kikanda. Utekelezaji wa Mpango huo unatarajiwa kuwa utasisimua uwekezaji na kuongeza nguvu mpya katika jitihada za kukuza mtangamano wa Bonde la Mto Nile na maendeleo ya watu wake.

Lengo la mikutano ya Baraza la Mawaziri ni kutoa maelekezo kuhusiana na masuala ya kisera kwa Sekretarieti na Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile.

# SUWASA Kuwatoa Kiu Ulemo-Misigiri



*Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akikagua mradi wa maji wa Ulemo-Misigiri unaotekelezwa na SUWASA, mkoani Singida*

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) amekagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji wa Ulemo-Misigiri mkoani Singida.

Mradi huo ambao ulianza kutekelezwa mapema mwaka 2021 unatarajiwa kukamilika Agosti 23, 2022 na kwa sasa umefikia asilimia 94 ya utekelezaji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA).

Mradi huo unatekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) na utagharimu shilingi milioni 569.3 ambapo awamu ya kwanza ilihusisha uchimbaji wa visima vitatu vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita 41,158 kwa saa.

Shughuli zilizotekelezwa mpaka sasa ni Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 400,000 ambao umefikia asilimia 99, Ujenzi wa tanki (Sump) lenye ujazo wa lita 45,000 umefikia asilimia 96, Ujenzi wa vituo viwili vya mitambo ya kusukuma maji umefikia asilimia 100

Shughuli nyingine ni ununuzi na ufungaji wa miundombinu ya kuzalisha maji(lita 30,000 kwa saa na lita 17, 000 kwa saa) umefikia asilimia 100, Ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji yenye urefu wa mita 2,850 umefikia asilimia 99, Ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa mita 10,400 umefikia asilimia 100.



# Miradi ya maji 1029 kutekelezwa vijijini




Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1029 ya maji vijijini ambapo miradi 648 ni miradi inayoendelea kutekelezwa na miradi 381 ni mipya. Aidha, miradi 175 imepangwa kutekelezwa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mahundi amesema hayo wakati akieleza vipaumbele vya sekta ya maji jijini Dodoma kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Amesema wizara ina matumaini makubwa kufikia malengo kutokana na uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameonesha nia ya dhati ya kuhakikisha mama wa Kitanzania anatuliwa ndoo ya maji kichwani.

Kuhusu ubora wa maji yanayopelekwa kwa wananchi amesema kuwa Wizara kupitia maabara zake 17 za ubora wa maji nchini itaendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini kwa lengo la kuhakikisha watumiaji wa maji wanapata huduma ya maji yanayokidhi ubora.

> “Matumaini yetu ni kuhakikisha maagizo tuliyopewa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inafikiwa.”
>
> Mheshimiwa Mahundi amesema

Jarida Tando



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz